JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S.L.P 1951,

Simu: 027-2750885;

Nukushi:027- 2750889

Barua pepe: rbckilimanjaro@pccb.go.tz

Wavuti: www.pccb.go.tz

KILIMANJARO – APRILI, 2022

TAKUKURU KILIMANJARO YASISITIZA WATENDAJI KUTOBADILI MATUMIZI YA FEDHA BILA KUFUATA TARATIBU ZA SERIKALI.

Ninawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanahabari na wananchi wote wa mkoa wa Kilimanjaro.

Ndugu wanahabari,

Leo tumewaita ili kuwapatia taarifa ya utendaji kazi wetu kwa miezi mitatu yaani mwezi Januari, 2022 hadi Machi, 2022 pamoja na mikakati ya TAKUKURU Mkoa wa Kilimanjaro kwa kipindi cha Aprili hadi Juni, 2022

Ndugu Wanahabari,

UCHUNGUZI NA MASHTAKA:

Katika kipindi hicho cha miezi mitatu, TAKUKURU Mkoa wa Kilimanjaro tulipokea taarifa **mia moja na ishirini na tisa (129)** ambapo kati ya hizo, taarifa **Sabini na tisa (79) zilikuwa zinahusu makosa ya rushwa** na **hamsini (50) hazikuwa na uhusiano na makosa ya rushwa**, hivyo watoa taarifa walielimishwa na kuhamishiwa katika mamlaka nyingine ambazo zina mamlaka ya kushughulikia tuhuma hizo.

Kati ya taarifa 79 zilizohusu rushwa, taarifa zinazoendelea na uchunguzi ni 76 na Taarifa ambazo uchunguzi umekamilika na kupelekea kufungua kesi mahakamani ni 03.

Mchanganuo wa malalamiko yaliyopokelewa kisekta ni kama ifuatavyo;

S/Na.	**IDARA HUSIKA**	**IDADI YA TUHUMA**
1	ELIMU	10
2	SERIKALI ZA MITAA	08
3	POLISI	11
4	SEKTA BINAFSI	12
5	MAHAKAMA	04
6	ARDHI	11
7	NISHATI NA MADINI	03
8	AFYA	19
9	USHIRIKA	07
10	TAMISEMI	08
11	MIFUKO YA HIFADHI YA JAMII	03
JUMLA		**129**

Katika kipindi cha Januari - Machi 2022, kesi mpya zilizofikishwa mahakamani ni saba (7) na hivyo kufanya jumla ya mashauri thelathini (30) yanayoendelea mahakamani. Katika kipindi hicho Jumla ya mashauri matano (5) yalitolewa hukumu na Jamhuri ilishinda mashauri hayo yote.

Ndugu Wanahabari,

UFUATILIAJI MIRADI YA MAENDELEO

Mkoa wa Kilimanjaro ulipokea kiasi cha shilingi 3,091,266,845/= kutoka Serikali Kuu, kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kama ilivyofanywa katika mikoa mingine ya Tanzania, kwa mchanganuo ufuatao kiwilaya.

- Wilaya ya Mwanga ilitumia jumla ya shilingi 440,881,345/= kwa mchanganuo fuatao: kiasi cha shilingi 29,500,000/= kilitumika kwa ajili ya ujenzi wa darasa, ofisi ya mwalimu Mkuu na jiko la shule ya sekondari Nyerere na shilingi 411,381,345/= zilitumika kwa ajili ya ukarabati wa barabarara kwa kiwango cha changarawe kutoka Kisangara-Shighatini na Kila-Butu.
- Halmashauri ya wilaya ya Rombo ilitumia jumla ya shilingi milioni 242,350,500/= kwa ujenzi wa barabara ya Useri Parish hadi Msangai kwa kiwango cha changarawe.
- Wilaya ya Hai ilitumia juma ya shilingi 178,440,000/=kwa mchanganuo ufutatao: shilingi 80,000,000, kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 4 ya shule za sekondari, kiasi cha shilingi 80,000,000, ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum na shilingi 18,440,000 ukarabati wa stendi ya Bomang'ombe
- Wilaya ya Siha imetumia jumla ya shilingi 1,020,860,000/= kwa mchanganuo ufuatao: shilingi 167,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya wanawake katika Hospitali ya Wilaya, shilingi 250,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la OPD – kituo cha Afya Orkolili, shilingi 553,860,000/= kwa ajili ya ukarabati wa barabara DC- Karansi – Makiwaru.
- Wilaya ya Same ilitumia jumla ya shilingi 80,000,000/= katika ujenzi wa bweni la shule ya msingi Same.
- Katika Halmashauri ya Moshi vijijini miradi iliyofuatiliwa ilikuwa na thamani ya jumla ya shilingi 628,235,000/= kwa mchanganuo ufuatao: kiasi cha shilingi 161,000,000 zilitumika kwa ajili ya mradi wa maji Mkolowonyi, kiasi cha shilingi 427,235,000/= kwa ajili ya kukarabati wa barabara ya Uchira, Miwaleni, Kisangesangeni kwa kiwango cha changarawe na shilingi 40,000,000/= zilitumika kwa ajili ujenzi wa vyumba viwili vya shule ya sekondari Mrereni.
- Manispaa ya Moshi imetumia jumla ya shilingi 510,000,000 kwa mchanganuo ufuatao: shilingi 470,000,000/= ujenzi wa madarasa 8 ya sekondari karanga, jengo la utawala, vyoo na maabara na shilingi 40,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 2 ya shule ya sekondari Moshi.

Kupitia ufuatiliaji huu, TAKUKURU Mkoa wa Kilimanjaro ilibaini kuwapo na dosari mbali mbali katika miradi hiyo ya maendeleo kama ifuatavyo:

- TAKUKURU (W) ya Same imeokoa fedha za miradi ya maendeleo katika kata ya Gonja kiasi cha sh. 22,945,000/= kwa mchanaganuo ufuatao:
  - Kwamba kiasi cha sh: 4,445,000/= kiliokolewa katika ukarabati wa mradi wa maji wa Jumuia ya Watumia Maji Majumbani Kimambu – Gonja Maore.
  - sh: 4,000,000/= ziliokolewa katika ukarabati wa shule ya Msingi Maore baada ya mwalimu Mkuu kuzichepusha fedha hizo kwa kuweka katika akaunti yake binafsi.
  - sh. 14,500,000/= ziliokolewa katika ujenzi wa choo wa shule ya msingi Kanza zilizokuwa zimefujwa na watendaji.

- TAKUKURU (W) Mwanga ilifanikiwa kuokoa kiasi cha sh. 573,000/= kutoka kwa mshtakiwa Mary Lukas Mchome katika kesi namba 94/2018 na fedha hiyo ilingizwa kwenye akaunti ya Serikali.

- TAKUKURU (W) Hai iliweza kumdhibiti mkandara wa Halmashuri ya Wilaya ya HAI aliyefanya ukarabati wa stendi Bomang'ombe chini kiwango kwa kurudia ukarabati huo kwa gharama zake baada ya kuwa ameshalipwa kiasi chote cha fedha za mradi huo yaani sh. 18,400,448.00

Ndugu Wanahabari,

UCHAMBUZI WA MIFUMO

TAKUKURU mkoa wa Kilimanjaro ilifanya chambuzi za mifumo katika Idara mbali mbali za Serikali kama ifuatavyo;-

- TAKUKURU (W) Siha ilifanya uchambuzi wa mfumo kuhusu mianya ya rushwa katika ukusanyaji wa mapato ya tozo za maji katika maeneo yanayohudumiwa na bodi ya maji Lawate – Fuka.

- TAKUKURU (W) Same imefanya uchambuzi wa mifumo miwili.
  1. Umoja wa mawakala wa mabasi katika stendi kuu ya Same (KAKIWAKI)

2. Wakala wa serikali wa ufundi na umeme (TEMESA)

- TAKUKURU kituo Maalum-Holili imefanya uchambuzi wa mfumo katika Halmashauri ya Moshi vijijini kuhusiana na viashiria vya rushwa ya ngono na nyinginezo katika sekta binafsi.

Ndugu Wanahabari,

ELIMU KWA UMMA

TAKUKURU Mkoa wa Kilimanjaro imeendelea kufanya juhudi za uelimishaji umma kwa lengo la kuwashirikisha wananchi kwenye mapambano dhidi ya rushwa ambapo kwa kipindi tajwa tumefanya Semina (18) katika Idara mbalimbali, mikutano ya hadhara (12), tumeimarisha klabu za wapinga rushwa (34),Maonesho (2) na pia tumeendesha vipindi vya Radio (6).

Vile vile, tulitayarisha makala (08) kwa ajili ya machapisho ya uelimishaji umma yanayoandaliwa na TAKUKURU. Aidha, katika kipindi Januari hadi Machi 2022, TAKUKURU INAYOTEMBEA ilifanikiwa kukutana na wananchi wa soko la Mitumba Maimoria katika Manispaa ya Moshi na kusikiliza kero zao mbali mbali na katika wilaya ya Rombo walifanikiwa kuwafikiwa wananchi wa soko la Mashati na wananchi na kusikiliza kero zao mbali mbali.

Ndugu Wanahabari,

USHIRIKIANO NA SKAUTI

Katika kipindi husika, TAKUKURU kwa kushirikiana na SKAUTI waliweza kutoa elimu ya madhara ya rushwa na jinsi wanachama wa skauti wanavyoweza kupambana na rushwa kwa jamii. Mafuzo hayo yalifanyika kwa walimu walezi wa Skauti katika halmashauri zote za Mkoa wa Kilimanjaro za Same, Mwanga, Rombo, Siha, Hai na Moshi.

MWELEKEO WETU APRILI-JUNI 2022

Ndugu Wanahabari,

Mwelekeo wetu katika kipindi cha mwezi wa Aprili - June 2022, tutaelekeza nguvu zaidi katika KUZUIA RUSHWA kwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna wanavyoweza kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kupitia vijana wa skauti na kupitia klabu za wapinga rushwa. Na pia tutashiriki katika kukimbiza mwenge wa Uhuru ambapo katika mwenge wa uhuru kunakuwa na ujumbe wa mapambano dhidi ya rushwa.

Vileile, tutafuatilia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ili kuhakikisha miradi yate katika kiwango bora kulingana na thamani ya fedha (value for money) na kwamba fedha zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Aidha tumejipanga kufanya chambuzi za mifumo katika Sekta za Afya, Maji, Ujenzi, Ukusanyaji wa Mapato, Ununuzi wa Umma, Nishati na Madini, Viwanda na Biashara pamoja na Uwekezaji.

Ndugu Wanahabari,

WITO

TAKUKURU mkoa wa Kilimanjaro inatoa wito kwa wananchi wote, kuendelea kutoa ushirikiano ili kuondoa kero za Rushwa katika jamii, kwani rushwa ni adui wa haki na adui mkubwa wa maendeleo. Hivyo kazi iendelee!

Imetolewa na,

Frida Wikesi
Mkuu wa TAKUKURU
Kilimajaro
0738150110